



# KIBABII UNIVERSITY

## UNIVERSITY EXAMINATIONS

2021/2022 ACADEMIC YEAR  
FIRST YEAR SECOND SEMESTER

### MAIN EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF MASTER OF ARTS IN KISWAHILI

COURSE CODE: SWA 823

COURSE TITLE: UTAFITI KATIKA SEMANTIKI NA PRAGMATIKI

DATE: 25/05/2022

TIME: 9:00AM-12:00PM

---

#### MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee. Kila swali lina alama 20.

MUDA: Masaa Matatu (3)

KIBU observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

**Maswali**

1. Licha ya dai kuwa semantiki na pragmatiki ni matawi ya lugha na isimu ambayo hayajakua na kupanuka kama zilivyo taaluma zingine za isimu, hatua madhubuti zimepigwa kuhusu utafiti katika nyanja hizi mbili. Fafanua. (alama 20)
2. Uundaji wa maneno yaliyokamilika na yenye maana katika lugha hutokana na mchakato unaohusisha ushirikiano wa vijenzi vya kategoria mbalimbali. Jadili. (alama 20)
3. Kazi kuu ya lugha ni kusahilisha mawasiliano kupitia upangaji ujumbe unaoeleweka na wenye maana (Habwe na Karanja, 2004). Jadili nafasi ya leksikografia katika taaluma ya semantiki. (alama 20)
4. Hakiki nafasi ya nadharia ya kitendo uneni katika taaluma ya pragmatiki huku ukibainisha sifa za tamko la kutenda na taratibu zinazohitajika ili tamko liwe kitendo neni. (alama 20)
5. Maneno katika lugha yoyote iwayo hubadilika na kupanuka kimaana. Fafanua visababishi na aina mbalimbali za mabadiliko haya ya kisemantiki katika lugha. (alama 20)